# MKATABA WA KUUZIANA ENEO

**KATI YA**

**DANKAN HERI MWIKWA (MSIMAMIZI WA MIRATHI YA HERI MWIKWA KABIRI)**

**NA**

**TANLAKE SAMAKI LIMITED**

---

**MKATABA WA MAUZIANO YA ENEO LILICHOPO ENEO LA KIMBWELA NCHI KAVU MPAKA ZIWANI AMBALO HALIJAPIMWA NDANI YA MKOA WA KIGOMA**

---

**UMEANDALIWA** NA WAKILI,
MICHAELMWANGATI (0762906069)
BARABARA YA LUMUMBA KARIBU NA KITUO CHA AFYA YA UPENDO
S.L.P 1091,
**KIGOMA.**



MICHAEL MWANGATI Tel: 0762906069 Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths macngati83@gmail.com P.O. Box 46012, Dar es Salaam

ae

# MKATABA WA KUUZIANA ENEO

Mkataba huu umefanyika hapa Kigoma leo tarehe ..30...... Mwezi...10..., 2021

**Kati ya**

**DANKAN HERI MWIKWA** (Msimamizi wa Mirathi ya Heri Mwikwa Kabiri), ambae katika Mkataba huu atajulikana kama **'MUUZAJI'** neno ambalo litawahusu mwenyewe, warithi wao, mawakala wao, na yeyote ambaye atakuwa anadai haki katika mkataba huu kupitia wauzaji.

**Na**

**TANLAKE SAMAKI LIMITED,** Hii ni Kampuni iliyosajiliwa kwa Sheria za nchi ya Tanzania ikifanya shughuli zake ndani ya Manispaa ya Kigoma mjini na Mikoa mingine ndani na nchi ya Tanzania, ambao katika Mkataba huu watajulikana kama **'WANUNUZI.**

**KWA KUWA;**

A: **Muuzaji ni Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Mzee Heri Mwikwa Kabiri** ambaye ndiye alikuwa mmiliki halali wa Eneo lililopo Kijiji cha Kimbwela ndani ya Mkoa wa Kigoma, eneo ambalo baada ya kukadhi limekuwa likitumiwa na Watoto wa Marehemu kwa kuishi na kwa shughuli za Kilimo.

B: **WAUZAJI** Wameamua kwa hiari yao kuuza eneo hilo tajwa hapo lenye ukubwa wa hekari Ishirini na Tano NUKTA Tatu Saba (hekari 25.37) na wanunuzi wamekubali kununua kiwanja hicho toka kwa wauzaji tajwa hapo juu.

C: **WANUNUZI ,** Wamelikagua eneo hilo na kwa ridhaa yao wamekubali kununua eneo hilo na wamejiridhisha kwamba eneo hilo halina Mgogoro wowote juu ya Umiliki wake.

**MKATABA HUU UNATHIBITISHA IFUATAVYO:**

1. **kwamba, MNUNUZI** amekubali kununua eneo hilo lenye Ukubwa wa hekari 25.37 kwa bei ya shilingi Laki Sita na Elfu Hamsini kwa kila hekari **(650, 000/=)** tu ikiwa ni bei halali ya eneo hilo kwa hekari moja.

2. **Kwamba,** wauzaji na wanunuzi wamekubaliana kwamba ndani ya eneo hilo kuna maeneo ambayo muuzaji anayefahamika kwa jina la Dankan Heri Mwikwa aliyauza kwa watu wengine, hivyo watu hao wametambuliwa na Mwenyekiti wa serikali ya Kijiji akishirikiana na bwana Dankan Heri mwikwa mwenyewe na siku ya kusaini kwa Mkataba huu watapewa kila mmoja kiasi cha shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini (250,000/=) kila mmoja mbele ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Kimbwela na watasaini nyaraka maalumu kwamba hawana madai yoyote ndani ya hekari hizo Ishirini na Tano nukta tatu Saba (25.37).

3. **Kwamba, MNUNUZI** amemlipa **MUUZAJI** kiasi chote cha makubaliano ya manunuzi ya eno hilo ambacho ni shilingi **Milioni Kumi na Sita na Laki Tano (16,500,000/=) hivyo mnunuzi hana deni.**



MICHAEL MWANGATI
Advocate
Notary Public & Commissioner for Oaths
mwangati83@gmail.com
P.O. Box 46012, Dar es Salaam

al

4. **kwamba, MUUZAJI** akishirikiana na ndugu zake ambao ni Mashahidi kwenye Mkataba huu wamekiri kuwa eneo hilo halina mgogoro wowote kuhusu umiliki wake na halijatumika kama dhamana ya mkopo katika taasisi za fedha.
5. **Kwamba, MUUZAJI** amemkabidhi **MNUNUZI** Eneo hilo na wameonyeshana Mipaka yote na Majirani hivyo hakuna Mgogoro wowote na majirani juu Mipaka ya eneo hilo na baada tu ya kufanya Manunuzi haya Mnuzi ataweka mipaka (Bicons) kwenye eneo lake.

6. **Kwamba,** Kuanzia tarehe ya kusaini mkataba huu eneo hilo tajwa hapo juu litakuwa ni mali ya **WANUNUZI** bila pingamizi yoyote ile nje ya Mkataba huu.
7. Kwamba, pande zote mbili za Mkataba huu zimekubaliana kuwa wale wote wanaokaa kwenye eneo hili watapewa muda wa siku thelathini (30 days) wawe wameshahama kwenye eneo hilo walilouza.

8. **Kwamba. MKATABA** huu unatawaliwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa yeyote atakaekiuka Masharti ya Mkataba huu, hatua za Kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa upande ule uliodhurika.
9. **kwamba,** Endapo mgogoro wowote utajitokeza sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatumika kutatua mgogoro huo.

Hivyo kwa ushuhuda wa Makubaliano haya pande zote mbili zinazohusika zimeweka

Saini katika mkataba huu leo tarehe ..30...... mwezi ....10...... 2021.



Mkataba umetolewa hapa Kigoma na kutiwa saini na **DANKAN HERI MWIKWA** Ambaye namfahamu binafsi/ ametambulishwa kwangu na ...—...................... leo tarehe 30...mwezi ..10....mwaka 2021

.............................

**MUUZAJI**

MICHAEL MWANGATI
Tel: 0762 ...
Advocate
Notary Public &
Commissioner
for Oaths
macngati83@gmail.com
P.O. Box 46012, Dar es Salaam

**SHAHIDI 01.**
**JINA:** MASUKEO BONIFAS, SHABANI
**SAINI:** ..........[signature]..........
**WADHIFA: MWENYEKITI WA SERIKALI YA MTAA**
**ANUANI:** ....332 KIGOMA.........

MWENYEKITI WA KIJIJI
KIMBWELA

**SHAHIDI 02.**
**JINA:** ........................
**SAINI:** ..........[signature]..........
**WADHIFA: MTENDAJI WA KATA**
**ANUANI:** S.L.P. 332 KIGOMA

AFISA MTENDAJI WA KATA
SIMBO

MASHAHIDI WENGINE AMBAO NI WANA FAMILIA

1. ONORINA HERY MWIKWA ........
2. KASHINDI HENRY MWIKA ........
3. JACKSON HERY MWIKWA ........
4. JUMA KHERI MWIKWA ........
5. ANTHONY BENJAMIN HONDRE ........
6. OMARY RAMADHANI MWIKWA ........

MBELE YANGU.

JINA MICHAEL MWANGATI

SAINI ______

WADHIFA WAKILI

ANUANI L091 KIGOMA

TAREHE 30/10/2021

MICHAEL MWANGATI Tel: 0762 906069 Advocate Notary Public & Commissioner for Oaths mcngari83@gmail.com P.O. Box 46012, Dar es Salaam

Mkataba UMETIWA **SAINI NA** umetolewa hapa **KIGOMA**

**TANLAKE SAMAKI LIMITED**

Ambaye namfahamu

binafsi/ ametambulishwa kwangu na ....—..............

leo tarehe 30...mwezi ..10.. mwaka 2021.

-TSL- TANLAKE SAMAKI P.O. Box 40936 LIMITED

.....................

MUHURI WA KAMPUNI



JINA Alexander Chetkovich

SAINI ......

WADHIFA Director

ANUANI P.O. Box 88 Kigoma.

TAREHE 30/10/2021.

JINA ..........................................

SAINI ..........................................

WADHIFA ..........................................

ANUANI ..........................................

TAREHE ______

MBELE YANGU.

JINA MICHAEL MWANGATI

SAINI ______

WADHIFA WAKILI

ANUANI L091 KIGOMA

TAREHE 30/10/2021

MICHAEL MWANGATI Tel: 0762 906069 Advocate Notary Public & Commissioner for Oaths mcngari83@gmail.com P.O. Box 46012, Dar es Salaam